



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUM

Dodoma, 09 Mei, 2023

Katika kikao chake cha tarehe 08 Mei, 2023, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na kifungu cha 19 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, Tume imewateua Madiwani Wanawake wa Viti Maalum watatu kujaza nafasi wazi za Madiwani katika Halmashauri tatu za Tanzania Bara.

Uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa Mujibu wa Kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292, akiitarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi za Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika Halmashauri tatu za Tanzania Bara. Nafasi hizo zimetokana na vifo vya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum wa Kata husika.

Madiwani Wanawake wa Viti Maalum walioteuliwa ni kama ifuatavyo:-

| NA. | JINA | CHAMA | HALMASHAURI YA |
|-----|-------------------------------|-------|-------------------------|
| 1. | Ndg. Sina Jamaldin Nyanga | CCM | Manispaa ya Lindi |
| 2. | Ndg. Mary Muhjimy Kombe | CCM | Wilaya ya Morogoro |
| 3. | Ndg. Mashavu Juma Barakabitse | CCM | Manispaa ya Kigoma Ujji |

Kailima, R.K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI